

UONGOZI



[Kundi la watoto waimba *Ile dini ya wakati wa kale*—Mh.]

Ikiwa ni zuri kutosha kwenu nyote, ni zuri kutosha kwetu nasi pia.

² [Ndugu fulani asema, “Sasa wanakukabidhi zawadi zao.”—Mh.] Jamani, hilo ni nzuri. [Watoto wanampa Ndugu Branham zawadi.] Asanteni. [Dada fulani asema, “Ni zawadi dogo tu, Ndugu Branham. Wale watoto waliweka mapeni yao na mahela. Na . . . ? . . .] Asanteni. Asante, ndugu yangu mdogo. Asanteni, watoto. Hakika nawashukuru, sana, sana. Na Mungu awabariki.

³ Mwajua, Yesu alisema, “Kadiri mlivyompa mmojawapo wa wadogo hawa, mmenitendea mimi.” Ninyi ni wanaume na wanawake wa kesho. Kukiwako kesho, mtakuwa.

⁴ [Nafasi tupu kwenye kanda. Kundi laimba wimbo mwingine—Mh.] Naamini ningehubiri kwa masaa mengi sasa, baada ya hayo yote. Nilikuwa naanza kuwaza nilikuwa naanza kuchoka. Si ajabu ninyi wasichana wadogo mwaweza kuimba vizuri sana, ninyi wasichana wadogo na wavulana; sikizeni jinsi dada zenu wakumbwa huimba na mama zenu, waimbaji ajabu. Hilo ni nzuri ajabu. Huyu msichana mdogo aliyeongoza wimbo huo ni nani, si ni wewe msichana yule mdogo niliyekutana naye ng’ambo pale? Hakika mna sauti nzuri; nyinyi nyote. Mli . . . naamini uimbaji mzuri sana niliopata kuusikia, ulikuwa papa hapa. Je, ninyi hujitunza wakati wote? [Ndugu fulani asema, “La. Hivyo ndivyo tuimbavyo.”] Vema, nawaambieni, ninyi—ninyi hakika mmebarikiwa na kuimba kuzuri sana.

⁵ Napenda kuimba kuzuri. Napenda tu uimbaji mzuri sasa. Mimi kila mara nilisema, nifikapo mbinguni nataka niwe wanapoimbia, na kusikiza. Singeweza kutosheleza shauku yangu ya nyimbo.

⁶ Mwajua kuimba huleta ushujaa. Mwajua hilo, sivyo? Wanajeshi, wanapoenda vitani, mwajua wafanyavyo? Wao huchoza muziki na kuimba, na kadhalika kuwapa ushujaa. Nasi tuendapo vitani, sisi huimba na—na hiyo hutupa moyo wa kuendelea.

⁷ Nawashukuru ninyi watoto kwa hiyo zawadi nzuri. Na ni . . . Bi. Branham, na kutoka kwa Rebekah, na Joseph, na Sara, na sisi sote, twawashukuruni sana. Ni vigumu kusema, jinsi ya kuwaambia hawa watoto wadogo, tukijua mlihifadhi mapeni yenu. Si—sitaki kuzichukua. Mwajua jinsi najisikia, sitaki kuzichukua. Bali nilitazama ndani humu nao walikuwa na noti ya dola kumu katika kadi hii, niliwaza, “Je, niichukue hiyo?” Niliwaza, “Naweza je kutenda hayo?”

⁸ Lakini nakumbuka hadithi fupi ninayowataka mjue. Siku moja kulikuwako mwanamke mjane, alikuwa na kundi la watoto, labda...baba wa hao watoto wadogo alikuwa ameaga dunia. Naye alikuwa tu na peni mbili. Naye alikuja kwenye njia za mji, wakati mmoja...Na ilikuwa ni pesa za fungu la kumi, mapeni tu kama ninyi nanyi nyote mlivyoweka, naye akazitumbukiza katika hazina ya Mungu. Yesu alikuwa amesimama pale, akimtazama. Nami nimeshangaa, “Ningefanyaje kama ningekuwa nimesimama pale?” Huenda labda ningekimbia pale na kusema, “La, la, dada usifanye hivyo. Hatu—hatuzihitaji sana hivyo. Unazihitaji kwa ajili ya watoto.” Mwaona? Sasa, singemwachilia, afanye hivyo. Lakini Yesu alimwachilia afanye hivyo. Mwaona, Yesu alimwachilia afanye. Kwa nini? Yeye ajua ni heri kutoa kuliko kupokea. Yeye alijua yale angemtendea, waona.

Kwa hivyo nawashukuru ninyi watoto wadogo kwa moyo wangu wote.

⁹ Nataka kushukuru kila mmoja wenu, kwa huu wakati mzuri wa ushirika, Ndugu Leo na Gene. Hizi zimekuwa siku tatu za kuabudu, kwangu mimi. Hata nje porini, ninapojaribu kujiachilia niende na kuwaza nilikuwa nikiwinda, mimi njia moja au nyingine, nawatazama na kusikiza mkiongea. Nami nilijaliwa adhuhuri hii kuzuru manyumbani mwenu. Sikuwahi kuona, kukiingia cho chote, nitakiita sijapata kuona nyumba nyingi safi na watu nadhifu, na walio na heshima sana kwa Kristo na Injili. Si—sikuwahi kuona hayo po pote. Nanyi hakika mlianzia kwa njia zuri, endeleeni tu na Mungu atakuwa pamoja nanyi. Nami yanipasa niwaone baadhi yenu. Niliona, majuzi, hawa dada, hata siwajui, kwa sababu yote yale ningea yangekuwa tu ni macho na mapua yao, nje chini ya zile shela. Na sasa naamini nawajua vema sana kupitia kwa ukarimu wa Ndugu Leo na Gene. Walionizungusha hapa na pale na kutembea nyumbani mwenu; na kusalimiana kwa mikono na—na watoto wadogo, manabii wa kiume na wa kike wa kizazi kijacho, kukiwako kizazi kijacho.

¹⁰ Mwajua, Yesu huwapenda watoto wadogo. Mwajua, yeye awapenda. Na kulikuwako na mvulana mdogo, wakati mmoja, aliyeitwa Musa, tutaongea habari zake kwa wakati mchache ujao. Naye alikuwa mwema...mwajua nini kilimfanya, nini kilimsaidia kumfanya mvulana mzuri? Yeye alikuwa na mama mzuri wa kumlea. Mwaona, hiyo ndiyo sababu. Yeye alimfundisha kuhusu Bwana. Nanyi wavulana wadogo na wasichana mna mama wa namna hiyo kuwalea, kuwafundisha kuhusu Bwana. Watiini tu.

¹¹ Mwajua nini, mwajua Amri ya kwanza katika Biblia, Amri ya kwanza iliyo na ahadi, iliyo na ahadi? Huenda ni vigumu kidogo kwenu kufahamu Amri hizi. Amri ya kwanza ni, “Usiwe na miungu mingine ila yeye.” Lakini Amri kuu...Na Amri

ya kwanza iliyo na ahadi kwayo, mwaona, ni kwa watoto. Je, mlijua hilo? Mwaona, yeye alisema, “Watoto, watiini wazazi wenu, ambayo yaweza kuzidisha siku zenu duniani, ambazo Bwana Mungu wenu amewapa nyinyi.” Kuwatii wazazi wenu na mtende mnayofanya, huenda ikawapa maisha marefu duniani, mliyopewa na Bwana, wakati mwingi wa kumtumikia.

¹² Natumai, leo, kuwa natazama kundi la wahubiri na waimbaji na wainjilisti wa siku zijazo, kama kunazo siku baada ya zetu.

¹³ Na kuna kitu kimoja pekee juu hapa, ninyi—ninyi humwua mtu kwa ukarimu. Mimi nilikula hata nisiweze kula, nami—nami sikuwahi kukirimiwa sana hivyo. Kama ningalikuwa malaika, niliyeshuka toka mbinguni, singekirimiwa vema zaidi ya hapo. Jambo pekee niwezalo kuwaambieni ninyi, ni, “Asanteni.” Na muwapo kule chini Tucson, huenda nisiweze kuwakirimia ninyi vizuri hivyo, kwa sababu sijui vipi; sijazoea kufanya hivyo, lakini nitajaribu vema niwezavyo. Karibuni.

¹⁴ Ndugu na Dada Shantz, nataka niwashukuru. Nami nilijaliwa kukutana na bintio na mwanao mdogo na mzuri, adhuhuri hii. Na—na kwa kuturuhusu sisi kutumia nyumba yake hapa huru kwa ibada. Kulikuwa na mambo kama hayo yaliyokuwa yakitendeka siku za Biblia, mwajua; kuwa Injili ilikuwa... Najua laonekana dogo sana. Sisi, sisi tundedhani hivyo. Lakini hili ni sawa kwa Mungu... Kwa Mungu, kama ilivyokuwa katika siku hizo.

¹⁵ Kumbuka, kama kungekuwa na miaka mingine mingi, wangetazama nyuma hapa na kusema, “Laiti ningaliishi tu katika siku zile kule Prescott! Laiti ningaliishi tu...” Mwaona? Sasa tunaishi katika siku hizo. Mwaona? Ndipo tunafikia kikomo chetu, kisha tunangoja thawabu yetu katika hiyo siku kuu.

¹⁶ Sasa tutafungua Neno la Mungu na kusoma. Lakini kabla hatujafanya hivyo, hebu tuongee naye kwa muda mchache.

¹⁷ Yesu mpendwa, siwezi kueleza ku—kujisikia kwangu na shukrani zangu kwa Ndugu Mercier, Ndugu Goad, na watu hawa wote wazuri na watoto wao wadogo, na jinsi wamekuwa wakarimu kwetu tangu tuwe hapa. Ukarimu ule unapita kila kitu tulichotarajia. Nasi twajua kuwa wao walikuwa wapendwa sana na wazuri. Lakini hatukujua kuwa tungekirimiwa kwa fahari hivi. Na, Bwana, naomba kuwa Uwepo wako kila mara utakuwa katika kituo cha watu hawa, Roho Mtakatifu atajaza kila moyo hapa, na utawapa Uzima wa Milele. Nasi tu, kama tunavyofurahia leo, na kuwe na siku isiyo na mwisho tutakapokutana uweponi mwa Yeye Ambaye tunamwabudu na kumpenda, na kutoa sifa zote kwa ajili ya vitu hivi. Hadi wakati huo, Bwana, tuweke waaminifu kwako na kwa Neno lako. Katika jina la Yesu twaomba. Amina.

¹⁸ Sasa, niliwawekeni ninyi sana asubuhi hii, nitajaribu kuharakisha sana aduhuri hii, na niongee katika njia ambayo huenda ikawa watoto wadogo, na watu wazima watafahamu, pia.

¹⁹ Nataka kusoma A—Andiko hapa, linalopatikana katika kitabu cha Mt. Marko, nami nataka kusoma toka kifungu cha 17 cha sura ya 10 ya Injili ya Mt. Marko, sehemu moja.

Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?

Yesu akamwambia, kwa nini kuniita mwema? hukuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu.

Wazijua amri, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako.

Akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyatii (samahani) nimeyashika tangu utoto wangu.

Yesu akamkazia macho, akampenda, kijana huyu, akamwambia, Umepungukiwa na neno moja. Enenda ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuata.

Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

²⁰ Sasa kwa watoto, na kwa watu wazima na wote, nataka kuufanya huu ujumbe mdogo umalizike kwa wakati wake, na upesi niwezavyo. Nami nataka kuchukua maneno yenyewe, “Unifuata,” nami nataka kuchukua somo *Uongozi*. Kufuata, na mtu mwingine kuongoza; *Uongozi* na “Unifuata.” Watoto wadogo, kile. . .

²¹ Kumbuka kuwa, hatua ya kwanza ambayo ye yote wetu alipata kupiga, mtu fulani alituongoza. Enyi kina mama mnakumbuka zile hatua za kwanza kijana na msichana mdogo walipiga, hawazikumbuki tena. Lakini mtu fulani aliwaongoza kwa hatua zenu za kwanza. Nakumbuka Billy Paul alipopiga hatua yake ya kwanza. Joseph na wengineo, walipopiga hatua zao za kwanza.

²² Kwa kawaida mama ndiye amwongozaye mtoto kwa hatua yake ya kwanza, kwa sababu yeye yuko nyumbani hali baba yuko nje akifanya kazi, akijaribu kupata riziki. Lakini, ni, wao hupiga hatua zao za kwanza. Na wakati wa usiku wanapoingia, baba, yeye kila mara yuasema. “Ee, baba,” bibi asema, “Yohana na Mariamu,” yule mvulana au msichana, “anaweza kutembea! Njoo uone!” Na hatua moja tu, huenda ilimbidi mama kumshikilia; ilimbidi kushikilia kidole cha mama, kwa sababu ulikuwa mdhaifu, na huenda uligeuka upande, wajua,

na kuanguka kidogo. Kwa hivyo ilikubidi ujishikilie kwa mkono wa mama, ili upige hatua yako ya kwanza.

²³ Sasa, mtu fulani alikusaidia, ulipopiga hatua yako ya kwanza. Na hatua yako—yako ya mwisho utakayowahi kupiga katika maisha, mtu fulani atakuwa akikuongoza. Unaona, naam. Nawatakeni ninyi mkumbuke hilo. Hatua yako ya kwanza, mtu fulani alikuongoza. Na hatua yako ya mwisho, mtu fulani atakuwa akikuongoza.

²⁴ Yatupasa tuongozwe. Mwajua, Mungu alitufananisha na kondoo. Na je, mlijua kondoo hawezi kujiongoza mwenyewe? Yeye ataenda mbali na apotee, naye—yeye hawezi kujiongoza mwenyewe. Naye yampasa awe na mtu fulani amwongoze. Na wakati mwingine. . . Mchungaji ahitajika kuongoza kondoo. Sasa hiyo ilikuwa nyuma kula katika siku za Bwana Yesu, Yeye alikuwa mchungaji mwema aliyeongoza kondoo.

²⁵ Lakini leo, mwaona, tunaishi katika siku nyingine, kila kitu kimebadilika na kupotoshwa. Mwajua mtu gani awaongozaye kondoo siku hizi? Mbuzi. Nanyi mwajua anakowapeleka yule mbuzi? moja kwa moja machinjioni. Hao kondoo wadogo hawajui wanakokwenda, kwa hivyo mbuzi huenda kwa—kwa zizi, pale machinjioni, na kondoo hajui zaidi kuliko kufuata kiongozi, kwa hivyo anawaongoza wao moja kwa moja hadi machinjioni. Na ndipo mbuzi yule huruka mtego, na kondoo huingia na kuuawa. Mwaona, mbuzi, ni kiongozi mbaya.

²⁶ Lakini Yesu Mchungaji Mwema Aliyewaongoza kondoo, Yeye aliwaongoza uzimani na kushika mikono yao. Mnaona, lakini mtu fulani apasa kuwaongoza kondoo.

²⁷ Ya kwanza ni upendo wa mama, halafu neno la baba. Baada ya mama kukupa wewe hatua ya kwanza, kisha unamtazamia baba yako, sisi sote, kwa hekima, kwa sababu yeye ni kichwa cha nyumba. Naye kawaida. . . Si kuwa yeye yu mwerevu sana, bali yeye—yeye amefanywa tu kiongozi wa jamaa yake, kwa hivyo twafuata yale baba yetu asemayo tufanye. Yeye asemapo, “Sasa, mwanangu, ningependa wewe utende jambo fulani na fulani,” ndipo tunamsikiza yeye kwa sababu ni hekima. Lakini sikiza, waona, yeye amejifunza chungu nzima nasi yatupasa tunuulize yeye, kuona yale yeye alijifunza na ndipo tunaweza kufaidika kwa hayo, ambaye amejifunza. Yeye hutwambia, “Sasa usiende na kufanya hili, kwa sababu nilifanya hilo. Baba yangu aliniambia nisilifanye, lakini nililifanya, na ilisababisha hili kutendeka, kitu fulani kibaya.” Kwa hivyo, mwaona, tuta. . . Ndipo yeye, baba, atwambia jinsi ya kutenda, na jinsi ya kutenda kweli.

²⁸ Ndipo baada ya mama kutuongoza, hadi wakati tumepata hekima dogo, kufahamu, toka kwa baba, ndipo tunapata mwingine. Tunapata kiongozi mwingine, na huyo ni mwalimu, mwalimu mzuri wa shule. Yeye ajaribu kuwafundisha na kuwapa

ninyi elimu, ya kukufaa vyema maishani, mahali fulani, kiwango uwezacho kusoma Biblia yako na kusoma nyimbo, na kujifunza juu ya Mungu na kusoma, mwenyewe. Mwaona? Ndiposa, jambo lingine, huenda ungekuwa na biashara, na mtu fulani akuandikie barua, mama, baba, mtu fulani akuandikie barua, hungeisoma. Waona? Kwa hivyo mwalimu, yuko nawe, naye akuongoza wewe ku—ku—kujifunza kuandika na kusoma. Na ni jambo nzuri, mwalimu mzuri, kukufunza vyema. Lakini sasa baada ya wewe kuacha hayo, wewe, baada ya kuacha mwalimu, mwalimu mmoja baada ya mwingine, toka kwa shule dogo ya msingi, darasa la kwanza, kuendelea hadi umalize shule ya sekondari au kuenda chuoni. Ndipo umalizapo chuoni, ndiposa mwalimu amekoma kukuongoza wewe. Waona?

²⁹ Sasa, mama amekufundisha wewe kutembea, waona. Baba, amekufundisha jinsi ya kuwa na busara na kuwa mvulana mwema, na jinsi ya kujitunza na kuwa na tabia njema. Mwalimu amekufundisha elimu, jinsi ya kusoma na kuandika sahihi. Lakini sasa unamwacha baba, unamwacha mama, na unamwacha mwalimu, sasa yapasa mtu fulani akuongoze wewe tokea hapa na kuendelea. Sasa nani unayetaka akuongoze kuanzia hapa na kuendelea? [Mtoto asema, “Yesu.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Yesu angekuongoza wewe tokea pale na kuendelea. Sasa, hilo ni jibu zuri sana, zuri sana. Yesu akuongoza tokea pale na kuendelea.

³⁰ Sasa wamwona huyu kijana tunayeongea habari zake, yeye anaitwa yule kijana tajiri na mtawala. Sasa mtu huyu, alikuwa ameongozwa vema. Sasa, mama yake alimfundisha kutembea. Na mwaona, yeye alikuwa bado kijana, labda tu amemaliza shule ya sekondari, na kijana mashuhuri. Na kwa kufundishwa vema, labda alienenda vyema, na mengineyo, jinsi mamake alivyomfundisha.

³¹ Naye alikuwa kijana a—aliyefanikiwa, pia, kwa sababu, tazama, alikuwa tayari tajiri. Naye alikuwa tu ki—kijana, labda wa umri wa miaka kumi na minane, ndiyo tu amemaliza shule ya sekondari, naye alikuwa tajiri. Sasa, mwaona, alikuwa na mwalimu mzuri, amfundishe aenende vema. Naye alikuwa na mwalimu mzuri, baba yake; hata ikawa hata alipokuwa yungali kijana naye alikuwa—alikuwa tajiri wa pesa, alikuwa amejipatia pesa nyingi. Huenda hakika alikuwa... alikuwa mtawala, hata kwa umri ule, aliyefanikiwa sana. Mwaona? Na sasa yeye alikuwa na mwa—mwalimu aliyekuwa amemfundisha, alimfundisha yeye mambo mazuri, jinsi yeye angekuwa. Yeye alikuwa na elimu yake.

³² Basi mwalimu mwingine huyu kijana aliyekuwa naye, inategemea vile umelewa, bali huyu kijana alipata mafundisho ya dini nyumbani.

33 Sasa, watoto wengine, je mlijua kuwa watoto wengi ambao hawana mafundisho yo yote ya kidini nyumbani? Baba na mama zao hawamwamini Mungu. Na baba na mama zao hunywa pombe, huvuta sigara, hupigana, na hutembea-tembea, mmoja kwa mwingine, usiku, na mengineyo, na hawapikii watoto wao wa kiume na wa kike chakula cha jioni, na kadhalika. Je, hamna furaha mna baba na mama wazuri walio Wakristo halisi? Sasa, unapokuwa na watoto, je hutaki kuwa baba na mama wa aina iyo hiyo kama baba na mama walivyo? Unaona? Sasa, lakini hayo yote ni mazuri.

34 Sasa, huyu kijana alikuwa amekuwa nao, na alikuwa na mafundisho ya dini. Mnaona, hiyo ilikuwa zaidi ya yale wengine wao walikuwa nayo, kwa sababu hawana mafundisho ya kidini. Lakini huyu kijana alikuwa amepata mafundisho ya kidini, kwa sababu, waona, kwa sababu yeye alisema alitii Amri zile tangu alipokuwa mtoto.

35 Sasa ninyi nyote pia mna waalimu wa kidini wazuri, kila mmoja wenu. Nanyi wavulana na wasichana, ninyi nyote mlikuwa na waalimu wazuri, baba na mama zenu hapa katika kituo hiki, wana kila kitu unacho...kila kitu mkijuacho mnachohitaji, kuwafanya nyinyi kuwa wanaume na wanawake wazuri na halisi, mtumishi wa Mungu.

36 Kwa sababu, kumbuka, siku moja utakufa, au ugeuzwe na uingie mbinguni. Na ukifa kabla Kuja Kwake, utanyakuliwa kwanza. Je, ulijua hilo? Je, ulijua wale waliokufa...mama na baba wakifa mbele yako, na Yesu asije katika kizazi chetu, je mwajua haya, baba na mama, watafufuka kwanza, wametukuzwa, mbele yenu? Mwaona? Parapanda ya Mungu italia nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao. Tutabadilishwa hivyo. Yatupasa tukumbuke hilo ndilo jambo muhimu maishani. Mwafahamu sasa? Hilo ndilo jambo muhimu maishani, litupasalo kutenda, ni kujitayarisha kukutana na Mungu.

37 Sasa, dini pekee haitafaidi. Mwaona, huyu kijana mtawala hapa alisema, "Mwalimu mwema..." Sasa kumbukeni, kabla sijalisema. Yeye alikuwa amefundishwa kuenenda vema. Alikuwa na elimu zuri. Yeye alikuwa amefundishwa biashara. Naye alikuwa tajiri, na mtawala na alikuwa na dini. Lakini yeye alikabiliwa na shida nyingine. Nayo inatukabili sisi sote, Uzima wa Milele. Dini haitupi sisi Uzima wa Milele. Dini, ni kifuniko, bali haitupi Uzima wa Milele. Ijapokuwa, yeye alifundishwa na waalimu bora sana waliokuwepo, yeye alikuwa bado amepungukiwa na kitu fulani. Na kijana yule alikijua kwa sababu yeye alisema, "Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi Uzima wa Milele?"

³⁸ Sasa, ninyi, ninyi mnaamini Yesu ni Mungu, sivyo? Kwa hivyo alijua mawazo ya kijana yule, kwa hivyo alisema, “Zishike Amri.” Yeye alirudi tena kwa dini yake, kuona angesemaje kuihusu dini yake. Yeye alisema sasa, yaani “Ishike dini yako.”

³⁹ Yeye alisema, “Nimefanya hili tangu ujana wangu,” wavulana wadogo kama ninyi. “Mama yangu na baba, na kasisi, walinifundisha dini. Lakini najua, katika dini yangu, kwamba bado sina Uzima wa Milele.” Mwaona?

⁴⁰ Waweza kuwa mwema. Usiibe. Usivute sigara. Usidanganye. Usimdinganye baba na mama. Usiseme huo uongo wa kwanza, kwa sababu, ukisema mmoja ndipo ni rahisi kusema mwingine, waona. Lakini haikupasi kufanya hivyo. Usiseme uongo wa kwanza.

⁴¹ Je, wajua kuwa mwili wako haukuumbwa udanganye? Mwajua, wana mtambo sasa, u—umo kwenye neva zako. Wanaweza kuweka mshipi mdogo kuzunguka kiwiko cha mkono hapa, na waweke mmoja kuzunguka kichwa chako, na ndipo unaweza kusema pale, tuseme useme, “Mimi mi—mimi nilidanganya kuhusu hilo, lakini naweza kulisema kwa urahisi sana hata wa—wao wataamini ni kweli.” Nawe unaweza kusema . . .

⁴² Wangalikuuliza, “Je, ulikuwa mahali fulani, kama uliketi katika gari la Ndugu Shantz, hali Ndugu Branham akihubiri, Jumapili adhuhuri siku hii?”

Nawe ungesema, “La, bwana. Sikuketi pale. La, bwana.”

⁴³ Unajua yale huo mtambo wa kuchunguza uongo utasema? “Naam, bwana, uliketi. Naam, bwana, uliketi.”

Unasema, “Sikuketi.”

Utasema, “Naam uliketi.”

⁴⁴ Kwa nini? Kwa sababu uongo ni kitu kibaya mno. Mwili haukuumbwa useme uongo. Na ni kitu kibaya mno, hata hutatiza taratibu yote ya neva, unaposema uongo. Whiuu! Zikishatatizwa hivyo, utapata vidonda vya tumboni, kumea kuvu, vingekuua. Ndiposa uongo ni kitu kibaya, kwa sababu, mwaona, haikupasi kudanganya, kuiba, kutenda yo yote ya mambo haya.

⁴⁵ Sasa, kwa hivyo huyu kijana huenda alikuwa . . . hajakata kudanganya, kusema uongo, hakuwahi kuiba, naye alifahamu moyoni kuwa alihitaji Uzima wa Milele. Kwa hivyo yeye alisema, “Nifanyeje niupate?”

⁴⁶ Na Yesu anaonyesha hapa sasa kuwa dini haitampatia. Kwa hivyo yeye alimjibu moja kwa moja, na kusema, “Zishike Amri.”

⁴⁷ Naye alisema, “Bwana, nimefanya haya tangu nilipokuwa mvulana mdogo, au mtoto, tangu utoto wangu. Nimefanya haya.” Lakini yeye alijua hakuwa na Uzima wa Milele. Kwa hivyo

Yeye alisema basi, “Ukitaka kuingia Uzimani, Uzima wa Milele, ukitaka kuwa mkamilifu, basi nenda ukauze ulivyo. . .”

48 Mwaona, sasa, ni vizuri kuwa na pesa. Mwaona, ni vizuri kuwa na pesa, kuwa tajiri. Na kuwa mtawala, hayo ni sawa. Lakini ni—ni jinsi ufanyavyo uwapo hivyo, waona.

49 Yeye alisema, “Nenda, kauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, watu wale wasio na cho chote; basi njoo, unifuata, nawe utakuwa na hazina Mbinguni.” Lakini yule kijana alikuwa na pesa nyingi sana hata hakujua cha kuzifanyia. Sasa, oneni, yeye alikuwa mashuhuri sana, huyo kijana alikuwa.

50 Naye—yeye—yeye alikuwa amejitayarisha vilivyo kwa maisha, jinsi baba yake na mama, na makuhani na wengine wote, walivyomtayarisha, lakini bado yeye alijua alikuwa amepungukiwa na kitu fulani. Sasa nawazungumzia watu wazima. Yeye, yeye alijua alikuwa amepungukiwa na jambo fulani, naye hakuwa na Uzima wa Milele. Yeye alijua hivyo, Mwaona?

51 Dini haitaleta Uzima wa Milele. Taratibu, mwamsho, unajisikia kitu fulani; u—ungeogopa, na usikie kitu fulani. Waona? Kulia, hivyo ni vizuri; kupasa sauti, ni kuzuri; lakini hayo bado siyo huo, waona. Umekabiliwa na Uzima wa Milele.

52 “Unasema, Vema, nimekuwa tu Mbaptisti thabiti, Mmethodisti, au Mpresbiteria, au Mpentekoste.” Hilo bado si swali lile.

53 Huyu kijana alikuwa hivyo pia, yeye alifundishwa katika dini ya siku hizo, lakini yeye bado hakuwa na Uzima wa Milele kwa hivyo yeye alitaka kujua la kufanya. Yeye alikuwa ameongozwa kwa ufanisi, kwa Hili. Lakini alipokabiliwa nalo, alikataa kuelekezwa kwa Uzima wa Milele, au kuongozwa. Viongozi wake wengine walimshikilia sana hata yeye hakutaka kuyaachilia. Mwaona?

54 Sasa hilo ni jambo fulani kama lile Ndugu Branham analosema. Baadhi yake ni magumu sana kwenu. Mwaona.

55 Elimu ni zuri, yawapasa muende shuleni na msome. Mwaona, hiyo ni zuri, lakini hiyo haitakuokoa. Kuwa na pesa nyingi, hilo ni zuri, ungewalea watoto wako, uwape nguo nzuri na vinginevyo. Na kama vile baba na mama wameshawafanyia ninyi nyote kazi, na mengineyo. Hilo ni zuri, lakini hilo bado haliwezi kukuokoa. Waona? Au ungeingia katika chumba cha uchunguzi wa sayansi na ujifunze jinsi ya kuweka vitu mbalimbali pamoja, au kutenganisha atomu, au vyo vyote wafanyavyo na—na uingie katika ro—roketi na—na uende mwezini, lakini hilo haliwezi kukuokoa.

56 Yakupasa ukabiliwane na kitu kimoja, Uzima wa Milele, na kunaye mtu mmoja pekee awezaye kukupa huo. Mama hawezi kukupa wewe. Baba hawezi kukupa wewe. Mchungaji wako

hawezi kukupa. Kiongozi wako hapa hawezi kukupa. Kila mtu anayepokea Uzima wa Milele yampasa aje kwa Yesu Kristo. Yeye ndiye wa pekee awezaye kukupa fungu hilo.

⁵⁷ Mwalimu wako aweza kukupa elimu, aweza kukufundisha; yakupasa ujifunze. Mama ya—yako aweza kukufundisha kutembea; yakupasa ujifunze kutembea. Baba yako aweza kukufundisha jinsi ya kuwa mfanya biashara, au kipi, yakupasa ujifunze hayo lakini ni Yesu pekee awezaye kukupa Uzima wa Milele. Waona?

⁵⁸ Kasisi wako, kiongozi wako, au wengineo, wanaweza kukufundisha dini yako, unaweza kujifunza Ujumbe tunaajaribu kufundisha, lakini bado hilo halitakupa wewe Uzima wa Milele. Yakupasa umkubali Mtu, Yesu Kristo. Mwafahamu hilo, ninyi nyote? Yawapasa kumkubali Mtu, Yesu Kristo, kupata Uzima wa Milele sasa. Lakini wakati mwingine uongozi mwingine huwa na ushawishi mwingi sana juu yetu hata hatujui la kufanya basi wakati hu—huo ufikapo.

⁵⁹ Sasa, ni jambo baya jinsi gani kukataa uongozi kufikia Uzima wa Milele, kwa sababu, waona, Uzima huo ni usioweza kukoma kamwe. Sasa elimu hiyo ni zuri, hiyo inatusaidia hapa. Biashara, hiyo ni zuri. Pesa, hizo ni nzuri. Kuwa mvulana mzuri na msichana, hilo ni zuri. Lakini, mwaona, maisha yaishapo hapa, imekwisha. Mwafahamu? Ninyi watu wazima mwafahamu? [Makutano wasema, “Amina.”—Mh.] Mwaona, imekwisha. Lakini basi yatupasa kumkubali Yesu Kristo, kwa ajili ya Uzima wa Milele. Yesu pekee anaweza kukuongoza kwenye huo.

⁶⁰ Na ijapokuwa, mwaona, huyu kijana alikuwa amepata vitu hivi shuleni, na kwa wazazi wake na kila kitu, yeye—yeye alipoteza kitu kikuu sana ambacho angalikuwa nacho, uongozi wa Roho Mtakatifu, maana Yesu alisema, “Njoo, unifuata.”

⁶¹ Nanyi wasichana mnaotoka tu shuleni, ninyi mtakaomaliza shule labda, baadhi yenu, hivi punde, nanyi wavulana; uongozi mkuu sana uliopo ni Yesu Kristo, maana huo ndio huongoza kuelekea Uzima wa Milele. Sasa, huu Uongozi humkabili kila mwanadamu, wanapewa nafasi kuchagua.

⁶² Na hilo ndilo jambo moja kuu tulilo nalo maishani, ni kuchagua. Siku moja. . .mwajua, baba na mama, walichagua kuwa na mtoto mdogo mzuri wa kiume na wa kike, kama ninyi—ninyi nyote mlivyo.

⁶³ Ndipo ninyi—ninyi mna haki, baada ya kitambo kidogo, kuchagua kama mnataka kujifunza kutoka kwa mwalimu, au la. Mwalimu anaweza kukufundisha, lakini unaweza tu kuwa ki—kijana mdogo mbaya, husomi; msichana mdogo mbaya, husikizi kamwe. Waona, una—una chaguo kufanya hivyo, ungali u mdogo.

Na mama aulize, “Je, ulipata A zo zote katika kadi ya ripoti yako?”

“La, nilifanya vibaya sana.” Unaona, sasa unaweza . . .

64 Mama aulize, “Sasa yakupasa usome.” Na yakupasa ufanye hivyo basi, uendelee kusoma kama mama alivyokuambia, kama baba alivyokuambia. Unaona, yakupasa usome.

65 Lakini una chaguo, unaweza kufanya hivyo au usifanye. Unaweza kusema, “Sitaki.” Unaona, una chaguo.

66 Baada ya kitambo kidogo utakuwa na chaguo la msichana yupi utakayemwoa, mvulana yupi atakayekua.

67 Una chaguo kila mahali maishani. Na ndipo una chaguo, tena, kama unataka kuishi baada ya maisha haya; au uwe tu mtu mzuri, anayejulikana, mchezaji wa sinema, au mcheza dansi, au cho chote kile.

68 Na watazame hawa wasichana wadogo hapa wenye hiyo sauti nzuri, muda mchache uliopita, wakiimba, mtoto huyo ilimbidi kuzoeza sauti hiyo. Naye angekuwa mwimbaji katika mchezo, au mwimbaji fulani. Nasikia sauti hizi za wavulana wadogo hawa, wavulana hawa, mngekuwa kama Elvis Presley, mkiuza haki yenu ya mzaliwa wa kwanza. Oneni, hamtaki hilo. Mwaona, ni kipawa Mungu aliwapa ninyi, nanyi yawapasa mchague, mwaona, ni wapi mtakapotumikisha kipawa kile, kwa ajili ya Mungu, au kama mtakitumia kwa Shetani. Mwaona?

69 Ndugu Leo hapa, ndugu yenu, oneni, sasa yeye ana kipawa, kuja na kuwaongoza watu. Sasa yeye atakifanyiaje? Je, yeye ataingia katika biashara na kujifanya mwenyewe milionea; au yampasa aje nje hapa na kutengeneza nyumba ambamo watu wanaotaka kuja pamoja na kuwaleta ninyi nyote watoto wadogo? Mwaona, yakupasa uchague kile utakachofanya.

70 Kila mmoja wetu yampasa achague. Na imetukabili. Lakini sote tumekabiliwa na hili jambo moja: “Tutafanyaje kuhusu Uzima wa Milele? Tutaishi baadaye, au la?” Ndipo yatupasa tuje kwa Yesu, kupata huo. Nafasi ya kuchagua, hilo ndilo jambo moja Mungu alilotupa. Yeye hatushurutishi katika jambo lo lote. Yeye hutuachilia tufanye chaguo letu wenyewe. Kwa hivyo yakupasa si kulazimishwa, bali kufanya tu chaguo lako mwenyewe.

71 Sasa hebu tufuatilie hili, watu wazima nanyi nyote sasa, kwa dakika chache, na watoto, wote pamoja. Hebu tufuatilie huyu kijana, na chaguo alilofanya, na kuona lilikomwongoza.

72 Sasa, wasichana hawa wenye sauti hizo zuri, wavulana hawa. Sasa labda ukue na uwe na sauti ya kuimba. Sasa chukua tu hilo jambo moja, na ungeweza. Sasa wewe, mie, huenda siku moja ukawaza kuhusu hilo.

73 Mwamjua huyu kijana anayeitwa Elvis Presley? Mmesikia kanda zangu. Mmesikia jinsi nisivyomharibia sifa kijana yule,

lakini mvulana huyo alikuwa na nafasi ambayo ninyi nyote mnayo. Mwaona, na yale yeye. . . yeye alitambua angeimba. Na tazama yale yeye alifanya, jambo lile lile Yuda alilofanya, Yuda Iskariote, alimuuza Yesu. Yesu alimpa mvulana yule hiyo sauti zuri. Naye hufanyaje? Akageuka na kuiuza kwa Shetani. Mwaona, yampasa afikie kikomo chake. Mwaona? Yeye alikataa kutembea na Yesu.

⁷⁴ Sasa huyu kijana hapa, huyu kijana tajiri na mtawala, yeye alitenda jambo lile lile. Hebu tufuate na tuone yale aliyofanya. Bila shaka, akiwa mtu mkuu hivyo, labda kijana mwenye umbo zuri, nywele zake nyeusi zimechanuliwa upande, mavazi nadhifu. Wasichana walidhani, “Wee, huyu ni kijana mwenye umbo zuri!” Lo, wangewaza hivyo. Huenda yeye angewapungia mkono, nao wangecheza-cheza tena naye, na mengineyo.

⁷⁵ Naye alidhani yeye ni mtu mkuu, mtu, unaona, kwa sababu yeye alikuwa na umbo zuri, alikuwa kijana. Yeye hakuwa akitazama chini pale kwenye kikomo chake. Yeye alikuwa tu akitazama hapa. “Mimi ni kijana. Mimi ni wa kumpendeza. Mimi ni tajiri. Naweza kununua cho chote nitakacho. Naweza kuwachukua wasichana hawa, na, wee, wote wananipenda. Nao wanajua mimi ni mtu mkuu.” Na, oneni, yeye alikuwa na hayo yote. Alikuwa amefuata maagizo ya baba yake, na kila kitu. “Nami ni mwenye dini mno. Mimi huenda kanisani.” Na sasa yeye angefuata hayo, waona; mashuhuri sana, tajiri, na anayejulikana. Na, naye. . .

⁷⁶ Kama tu siku hizi, kama mlivyokuwa na nafasi kuwa mchezaji wa sinema, mwaona, au kitu kama hicho. Watoto wengi siku hizi, ongea nao, wanajua zaidi kuhusu hawa wachezaji wa sinema kuliko wanavyojua kuhusu Yesu. Mwaona? Na, oneni, ninyi—ninyi watoto mnajifunza kuhusu Yesu. Wanapoketi, na mchezo fulani unakuja kuhusu wachezaji wa sinema, au kitu fulani kinginecho, wanajua wachezaji na yote pale, na kila kitu. Wanajua hayo bora zaidi kuliko *Hiyo*. Uwaambie kuhusu Bibia, hawajui lo lote kuhusu Bibla. Unaona, ni kufanya chaguo mbaya, sasa. Baadhi ya waimbaji wanauza kipawa chao walichopewa na Mungu, kwa ajili ya sifa!

⁷⁷ Ndipo tunamwona yeye mwishoni mwa maisha. Hebu tumfuate zaidi kidogo. Mwajua yale Biblia husema huhusu huyu kijana? Yeye alifanikiwa zaidi. Kwa hivyo, wakati mwingine kufanikiwa hakumaanishi kuwa umefanya chaguo sahihi. Mwajua lile alilofanya? Yeye aliondoka na kuwa na wakati wa kujumuika, na kuandaa karamu kubwa kubwa, na kutumia pesa nyingi na kila kitu kwa wasichana na mengineyo. Na ndipo alioa na labda akawa na jamaa. Na—na yeye—yeye alifanikiwa sana hata akajenga maghala mapya na mengineyo. Naye alisema, “Mwaona, sikumfuata Yesu, na tazama vile nilivyo navyo!” Unaona?

78 Huenda ukawasikia watu wakisema hayo, nami nimewasikia, “Vema, tazama, yeye amenibariki.” Hilo halimaanishi cho chote. Waona?

79 Na baada ya kitambo kidogo maghala yalipopanuliwa hata yeye akasema, naam, hata, “Nafsi, starehe. Nina pesa nyingi sana na mafanikio mengi sana! Nami ni mtu mkubwa! Mimi nimo katika vyama vyote. Nami nina utajiri wa ulimwengu mikononi mwangu. Nina ardhi kubwa na pesa nyingi, na, naam, jamani, pale kila mtu ananipenda, mie nimekuwa mtu mwema sana.”

80 Lakini unajua Biblia ilisema ya kwamba usiku huo, Mungu alimwambia, “Nitaitaka nafsi yako.”

81 Ndipo kipi kilitendeka? Sasa kulikuwako mwombaji, maskini Mkristo mzee aliyelala pale mlangoni pake. Na ndipo walipo . . .

82 Kule Yerusalemu, kule juu, wao—wao hulia juu ya nyumba. Na makombo huanguka hivi, na vipande vya nyama, na kadhalika, huanguka sakafuni wanapovitupa. Nao hawaviokoti, kwa sababu kila kitu katika Yerusalemu, ule mji wa kale, ni—ni . . .

83 Ni vema kufanya mzaha mdogo hapa? Wao ni i-j-m, mwajua hilo ni nini? Inzi juu ya mkate, inzi juu ya nyama, inzi juu ya siagi, i-j-m, inzi juu ya kila kitu. Wanatoka kule kwenye njia za mji, mapipani na kote kote, na kuingia na kutua juu yake.

84 Kwa hivyo watu hawa juu pale, huenda juu ya—ya jengo. Nao hula, kisha makombo haya huanguka, ndiposa wao hufagia. Na mbwa, kwenye njia za mji, hula makombo yale. Naye alimwachilia huyu maskini Mristo mzee alale pale kwenye njia ya mji ale tu makombo yaliyoanguka toka kwa sahani yake toka kwa kitanda chake, au toka kwa meza yake.

85 Kisha yeye alipoingia, baada ya kitambo kidogo, akawa na vidonda, naye hakuwa na cho chote cha kufunga vidonda vyake. Jina lake lilikuwa Lazaro. Na mbwa wakaja na kuramba vidonda vyake ili ajaribu kupona.

86 Vema, mwajua, baada ya kitambo kidogo, huyu tajiri, wakati, alipoona yeye alikuwa na pesa za kununua kila aina ya madawa, kama angekuwa mgonjwa, alikuwa na namna zote za madaktari. Lakini, mwajua, wakati mwingine madaktari hawawezi kutusaidia, madawa hayawezi kutusaidia, hakuna cho chote kiwezacho kutusaidia. Sisi tuko chini ya rehema za Mungu. Naye alifikia kikomo cha safari yake; madaktari hawangemsaidia, na wauguzi hawangeweza kumsaidia, madawa hayangeweza kumsaidia, naye akafa. Na ndipo nafsi yake alipouacha mwili wake, mwaona, aliacha pesa zake zote, elimu yake yote, kila kitu ambacho alikuwa nacho, sifa zake zote. Wakamfanyia mazishi makuu mno, huenda bendera ilipepea nusu-mlingoti, na—na meya wa mji ule akaja, nao, na mhubiri

akaja na—na kusema “ndugu yetu sasa ameshaenda Utukufuni,” na yote kama hayo.

⁸⁷ Lakini Biblia ilisema, kuwa, “Aliinua macho yake kuzimuni, alipokuwa katika mateso, na kutazama kule ng’ambo ya hilo shimo kubwa pale, na kuona mwombaji yule aliyekuwa amelala pale mlangoni mwake, kule mbinguni. Naye alilia, ‘Umtume Lazaro hapa na maji kidogo. Moto huu unanitesa.’ Kasema, ‘Lo hapana.’”

⁸⁸ Oneni, yeye alichukua chaguo mbaya maishani; mwaona, alipofika mwishoni mwa safari, kuondoka maishani. Yeye alikuwa ameongozwa na dini. Alikuwa ameongozwa na elimu. Alikuwa ameongozwa na ushawishi wa ku—kufanikiwa kwake. Lakini, mwaona, yeye hakuwa na chochote cha kumshika mkono wake, mambo hayo huishia pale. Mwafahamu, watoto? Ninyi watu wazima mnafahamu yale ninayo. . . Yeye hakuwa na lo lote la kumshika. Pesa zake hazingemsaidia. Marafiki zake pamoja na madaktri hawangemsaidia. Madawa hayangemsaidia. Kasisi wake, dini yake, havingemsaidia. Kwa hivyo, kulikuwa na jambo moja pekee kwake kufanya. Yeye alikuwa—alikuwa amemkataa Yesu, Uzima wa Milele. Kwa hivyo ilimpa yeye atende nini? Azame mautini, kuzimuni. Ni kosa kuu jinsi gani kijana yule alilofanya alipokataa kuenenda na Yesu, kuongozwa na Yesu. Yeye alikataa kufanya hivyo.

⁸⁹ Vijana wengi sana wanafanya kosa hilo, siku hizi, kukataa kuongozwa na—na Bwana Yesu. Sasa, twaona ni kosa kuu jinsi gani kukataa Uzima wa Milele na kuongozwa na Yesu, Uongozi, Yeye aliposema, “Njoo, unifuate.”

⁹⁰ Mnaona yale huyu kijana mwenye umbo zuri aliyosema adhuhuri hii? Umalizapo shule, uondokapo, unahitaji kiongozi mwingine, hebu huyo awe Yesu. Na Yesu ni Biblia. Je, unaamini hilo? Huu ni Uzima wake Yesu na Amri zake kwetu, katika maandiko. Kwa hivyo yatupasa kuzingatia Hili, kuona. Hii ni ramani. Hii ni ramani ambayo yeye alituaambia tuiquate, ku—kuanza Uzima wa Milele.

Sasa twaona kuwa huyu kijana alipotea.

⁹¹ Sasa hebu tumchukue mwingine. Je, mngependa, mngekuwa na wakati kuchukua kijana mwingine tajiri mtawala, aliyepiga hatua njema? Je, mngependa kusikia hilo? Vema, tutajaribu hilo sasa. Hebu tuchukue kijana mwingine mtawala aliyekuwa tajiri aliyekabiliwa na jambo lile lile. Sasa twaona ambapo kijana yule alienda, aliyeishi maisha bora mno, lakini akafa na akapotelea kuzimuni, na sasa hapa tutaongea kuhusu kijana mwingine aliyekabiliwa na jambo lile lile. Yeye alikuwa tajiri, kijana na mtawala, na, lakini alikubali kuongozwa na Kristo; kama yule kijana alivyotuaambia muda mchache uliopita, ambaye inatupasa kumwachilia atuongoze. Yeye alikubali.

⁹² Maandiko ya haya yanapatikana, ukitaka kuyafungua nitakapomaliza, hapa, ni katika Waebrania, sura ya 11, na kifungu cha 23 hadi 29, Hebu niisome. Ni vema? Mtanivumilia kidogo nyote, sivyo? Hamtajali kufuatilia hayo, sivyo? Kwa hivyo tuta—tutasoma tu haya, ndipo msembe, “Nilimsikia Ndugu Branham akisoma hili toka kwa Biblia.” Mwaona? Nanyi mtajua yako basi. Si yale niliyoyasema, ni yale Yeye alisema. Sasa ninyi sikizeni hapa, yale Biblia ilisema hapa kuhusu huyu mtu mzuri. Mwaona. Sasa tazameni.

Kwa imani Musa, alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri, wala hawakuioogopa amri ya mfalme.

Kwa imani Musa alipokuwa . . . mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; (sikizeni)

Akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo;

Akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwa Kristo . . .

⁹³ Kule nyuma kabisa wakati wa Musa, ilikuwa bado ni Kristo. Mwaona? Yeye ndiye pekee aliye na Uzima wa Milele. Mnaona?

⁹⁴ “Akihesabu ya kuwa kushutumiwa” kuitwa aliyerukwa na akili, mtakatifu anayejigaragaza, au kitu kama hicho, mwajua. Mwaona?

Akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwa Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri, kwa kuwa aliyatazamia hayo . . . malipo.

⁹⁵ Sasa mwajua maana ya hayo? Yamaanisha haya, kwamba, Musa alizaliwa mvulana maskini, maskini sana. Jina la baba yake lilikuwa Amramu. Jina la mama yake lilikuwa Yakobeti. Nao walikuwa maskini mno, bali walikuwa Wakristo. Walifanya kazi kwa bidii. Walikuwa utumwani. Iliwabidi kutengeneza matofali, na kadhalika, kumtumikia yule mfalme wa kale. Mwajuaje? Huyu binti wa mfalme alishuka kwenda chini, siku moja, mtoni ambapo mama . . .

⁹⁶ Mama ya Musa, Yakobeti, alikuwa amemtwa na kumweka yeye katika kisafina kidogo mtoni hivyo. Na wale mamba wa kale walikuwa wamekula watoto wote wachanga; nao walikuwa wakiwaua, wakiwatupa mtoni. Lakini yeye alimweka nje pale. Nanyi mwajua jinsi alivyowafukuza mamba wale? Yeye alifanya hiki ki—kijisafina akamweka ndani, alikitengeneza kwa lami. Mwajua hiyo ni nini? Ni terafini. Mamba angekuja, tuseme, “M—mtoto Mwebrania mnene, nitamla!” Msikieni akilia hivyo. Akaenda pale, “M-m-m! Harufu jinsi gani! Eehei!” Mwaona? Mwaona, mama yule aliongozwa, jinsi ya kumlinda mtoto wake. Kwa hivyo huyo naye alikiacha akaondoka, hakutaka lo lote kuhusiana nacho.

⁹⁷ Na ndipo yeye akatelemka mtoni, mbali kidogo. Na dada yake mdogo, aliyeitwa Miriamu, alimfuata chini mtoni, akashika zamu.

⁹⁸ Na ndipo binti Farao akaja na alikuwa yuaenda kumchukua, mwajua, naye alimtoa nje. Mwajua, nyote... Mwajua, mama yako hufikiria wewe ndiye mtoto mzuri sana ulimwenguni; unaona, yeye angefanya hayo. Lakini Biblia ilisema, huyu mtoto mwanamume alikuwa wa kupendeza sana, mvulana mzuri mno. Na, lo, yeye alikuwa tu akilia na kupigapiga mateke. Yeye alikuwa amemkosa mama yake, mwaona. Na kwa hivyo mwajua nini kilitendeka? Ndipo Mungu aliweka binti Farao, yule binti mfalme, upendo wote ambao mama angekuwa nao kwa mtoto wake mchanga. Moyo wake ukampenda. Yeye kasema, "Huyo ni mwanangu."

⁹⁹ Lakini, mwajua, yeye alikuwa mwanamke kijana. Oneni, siku hizo hawakuwa na chupa hizi ambazo ninyi, watoto, mlizwa kwazo, kwa hivyo iliwapasa wampate mama aliyekwisha kuwa na mtoto, na kumpa huyo amlee.

¹⁰⁰ Kwa hivyo Miriamu alikuwa papo hapo kuwasaidia, naye kasema, "Nitaenda kukuletea mama anayefaa."

"Vema, nenda kamlete."

¹⁰¹ Mwajua Miriamu alienda na kumleta nani? Mama ya Musa. Naam. Basi, akaenda na kumleta. Hiyo ilikuwa hekima, sivyo? Na kwa hivyo basi alienda na akamleta mamake Musa. Naye alisema, "Nitamchukua na kukulelea huyu mvulana mchanga."

¹⁰² Yeye alisema, "Wajuaje, nitakulipa dola mia tatu, kwa juma, kumlea mtoto huyo. Nawe waweza kukaa katika jumba la mfalme." Oneni jinsi Mungu hufanya unapomtumainia, mwaona, unapokuwa na hakika ya imani. Huyo mtoto alikuwa nabii, mnaona, na mama alijua.

¹⁰³ Kwa hivyo walienda katika lile jumba la mfalme na—naye alimlea Musa, na mama yule, mama yake, akapata dola mia tatu, kwa juma, kwa matumizi yote. Waza tu kuhusu hayo!

¹⁰⁴ Na ndipo, mwajua, baada ya kitambo kidogo, baada ya hayo kuendelea kwa muda mchache, Musa akaanza kuwa mkubwa kutosha kusoma na kuandika. Yeye alimfundisha jinsi ya kusoma na kuandika. Na ndipo yeye alimwambia, kasema, "Musa, ulizaliwa mwana sahihi. Mimi na baba yako tumeomba. Mungu ametufunulia sisi kuwa wewe u nabii, nawe utawakomboia watu, siku zijazo."

¹⁰⁵ Nanyi mwajua alipokuwa mkubwa basi yeye alikuwa nani, alifanywa mwana katika jamaa ya mfalme. Jamani yeye haikumbidi ku... .

¹⁰⁶ Naye aliwatazama watu wake kule nje, nao hawakuwa na mavazi. Wao walikuwa Wakristo, nao walikuwa wakilia. Nao wale wasimamizi wakiwapiga kwa mijeledi, na damu ikitiririka

toka migongoni mwao. Binamu wa—wake na wajomba, baba na mama, hao wote; wakipigwa kwa mijelezi, nje pale katika hayo mashimo ya matope. Na kwa hivyo, lakini Musa, akiwa na kitu fulani moyoni mwake, alijua kuwa wao walikuwa watu wa ahadi wa Mungu. Yeye alijua hilo.

¹⁰⁷ Sasa, jambo la pili angalifanya ni kuwa mfalme. Yeye angekuwa mfalme juu ya kila kitu, mtu tajiri, jamani, pesa zote za misri. Na Misri ilitawala ulimwengu, wakati huo. Lakini, tazama, Biblia ilisema, “Yeye alihesabu kushutumiwa,” kuwa kama mkanyaga matope nje kule, Mkristo. Walipo wadhihakiki, na kuwachekelea, waliwapiga mateke. Wakijibu lo lote, waliwaua. Mwaona? Lakini Musa alichagua kuenda na kundi lile badala ya kuitwa mwana wa mfalme.

¹⁰⁸ Tazama hilo! Waona kwa sababu yeye aliona wakati wa mwisho! Mwone huyo kijana tajiri. Lakini yeye alimwona Yesu, kama tumwonavyo katika ono, kuwa wakati wa mwisho ndilo jambo muhimu. Sasa, naye alikubali uongozi wa Kristo, na Musa alihesabu kushutumiwa kule kuwa hazina kuu.

¹⁰⁹ Mwajua, wakati mwingine ninyi wavulana wadogo kule shuleni, wavulana wadogo watasema maneno maovu nao wanawatakeni ninyi nyote myaseme. Ninyi wasichana, wasichana watasema maovu na wanawatakeni ninyi nyote myaseme. Usemepo, “La, mimi ni Mkristo.”

¹¹⁰ Wao husema, “Aaa, mwoga mkubwa wee!” Mwajua, hukurukia hivyo.

¹¹¹ Waona, simama, useme, “Nina furaha kuwa hivyo.” Unaona? Kwa sababu, oneni, hayo ndiyo aliyofanya Musa. Yeye alihesabu kuwa kushutumiwa kwa Kristo ni utajiri mkuu kuliko Misri yote? Sasa, hebu tumfuate, akiongozwa na Kristo, na tuone yale yeye alitenda.

¹¹² Sasa, oneni, huyu kijana alikuwa tajiri, yule kijana wa kwanza, lakini yeye hakumtaka Kristo. Yeye hakutaka kuwa mfuasi wa Yesu. Na kwa hivyo twamwona yeye akiwa mashuhuri sana, labda akawa mchezaji wa sinema, na mkuu kwa vyote, katika yote yale—yale mambo aliyoweza kuyafanya, na kila kitu alichotaka. Lakini alipokufa, hakuwa na ye yote wa kumwongoza. Kwa hivyo, elimu yake, hiyo ilikuwa zuri, pesa zake, hizo zilikuwa zuri; lakini mauti ilipoingia, yote ilikwisha, yeye hangeitumia tena. Yeye hangejinunulia kuingia mbinguni. Naye hakuweza, kwa elimu yake, yeye hangeenda mbinguni. Mwaona?

¹¹³ Lakini huyu kijana sasa, yeye alikuwa na vitu hivi vyote. Alikuwa na elimu, pia, alikuwa mwerevu. Alienda shuleni, na mama yake alimfundisha, na—naye alikuwa na elimu zuri. Naye alikuwa mwerevu mno, hata ikawa angewafundisha Wamisri. Yeye alimfundisha mwalimu wake, yeye alikuwa mwerevu mno. Tazama jinsi alivyokuwa mwerevu. Lakini, mwajua nini, mbali

na huo werevu wote mbali na yote walivyokuwa nayo, zile nguvu alizokuwa nazo, yeye bado alisema, “Nitaviacha vyote, na kumfuata Yesu.” Mwajua yale waliyomtendea? Walimfukuza. Yeye akawa m—mtumwa matopeni kama wengine wote.

114 Lakini siku moja alipokuwa mtu mzima, alikuwa akichunga kondoo nyuma ya jangwa. Na nini kilitendeka? Mtu ye yote aniambie nini kilitendeka? Ilikuwa nini? [Mtoto fulani asema, “Kulikuwa na moto katika kijiti.”—Mh.] Naam, kulikuwa na moto katika kijiti, na Ulimvutia macho. Yeye aligeuka upande. Nanyi mwajua je?

115 Badala ya kuwafundisha watoto, sasa watoto watainuka na kunifundisha mimi. [Ndugu Branham acheka—Mh.] Kwa hivyo, na huyu mvulana mdogo hapa, yeye amelipata—amelipata sahihi. Baba yako ni nani? [Mtoto yule ajibu, “Bw. Shantz.”] Bwana shantz ni baba yako. Mvulana huyo amefundishwa, sivyo? Kila mmoja wao ana macho yanayong’aa yakiangalia vivyo hivyo, mmoja apate kutangulia mwingine, mwaona.

116 Kwa hivyo sasa tazama, yeye alijificha katika hicho... Na hicho—hicho kijiti kilimvutia, kikiwaka, naye alisema, “Nitageuka na nione ni nini.”

117 Na Mungu alimwambia Musa, “Vua viatu vyako, mahali unaposimama ni patakatifu. Nimekuchagua kuenda chini kule na kuwakomboa watu wangu. Ninakupa nguvu; unaweza kupiga nchi kwa mapigo, unaweza kuyageuza maji yawe damu, unaweza kuleta viroboti na chawa. Hakuna cho chote kitakachokudhuru. Nilikuchagua.” Kwa nini? kwa sababu yeye alimchagua Kristo. Mwaona? Unamchagua Kristo, na yeye anakuchagua. Waona? Sasa, Yeye alisema, “Ulinichagua mimi, nami nimekuchagua uende chini kule Misri.”

118 Na tazama yale aliyofanya, Yeye aliwaongoza watu milioni mbili, kuwatoa watu milioni mbili, watu wake, na kuwaingiza katika nchi ya ahadi. Na, sasa, yeye alifuata. Sisi tumfuate jangwani kote; nanyi watoto mmewasikia Ndugu Leo na Ndugu Gene, na baba na mama zenu wakiwaambia yale yaliyotendeka jangwani, jinsi yeye alivyoleta toka mbinguni mikate na kuwalisha watu wenye njaa, na mambo haya yote.

119 Na sasa tunaona yu mzee sasa, amezeeka sana, ana umri wa miaka mia na ishirini. Naye yuko jangwani.

120 Na hao watu hawakumtendea vema, hata hivyo. Mwaona, wakati mwingine watu wanaojiita wenyewe wakristo hawakutendei vema. Lakini yesu kila mara hukutendea vema. Unaona? Unaona? Kwa hivyo twaona sasa kuwa watu wale walimuasi, lakini yeye hakuwaacha, kwa vyo vyote. Naye alikuwa kiongozi, naye ilimbidi akae nao. Na malaika za Bwana waliongea naye. Haungependa hayo yatendeke kwako? Basi fanya chaguo lifaalo, na mchagua Yesu, naye atayafanya hivyo.

121 Sasa, ndipo twaona, mwisho wa safari, yeye akawa mzee sana. Hangehubiri tena, na sauti yake ikafifia. Kwa hivyo yeye akambariki Yoshua, na akaenda juu mlimani, akafe.

122 Mwajua yale yaliyotendeka yeye alipokufa? Pale, nini, nini kilitendeka? [Mvulana mdogo asema, “Yeye alikufa, na ndipo yeye akamfufua toka kwa wafu.”—Mh.] Ndivyo, hasa. Ndivyo hasa.

Sasa unasema, “Hayo yako wapi?”

123 Sasa, ngoja kwa dakika moja, mvulana huyu amepata, waona. Yeye alifufuliwa toka kwa wafu. Sasa, Miriamu najua ulijua hilo. Unaona? Sasa tazameni. Yeye alimfufua toka kwa wafu. Kwa nini? Kwa sababu, miaka mia nane baadaye, huyu hapa Palestina, bado akisimama na Kiongozi wake, Yesu, aliyehesabu ya kuwa kushutumwa kwa jina lake ni hazina kuu kuliko utajiri wote wa Misri. Yeye alihesabu. . . Kiongozi wake alikuwa amesimama pale. Mwajua, yeye alitwa . . .

124 Katika—katika Biblia, Mwajua, kulikuwa na mwamba uliowafuata Israeli. Na Musa alipokuwa tayari kufa, yeye alisimama kwenye mwamba huu. Na mwamba huo ulikuwa Yesu. Mwakumbuka Yesu alipokuwa akiongea, katika—katika Injili ya Yohana, mlango wa 6?

Vema, yeye alisema, “Baba zetu walikula mana jangwani!”

125 Kasema, kasema, “Baba Yangu aliwapa mana hiyo.” Yeye alisema, “Naam walikula mana. Hiyo ni kweli. Wamekufa, kila mmoja, wao kwa sababu hawangezidi kusonga mbele, mwaona.” Kasema “Wamekufa kila mmoja wao,” Lakini kasema, “Mimi ndimi chakula cha Uzima kilichotoka mbinguni kwa Mungu.”

126 “Baba zetu walikunywa kutoka kwa ule Mwamba. Musa alipiga mwamba ule,” na kasema, “na maji yakabubujika.”

Yeye kasema, “Mimi ndimi Mwamba ule uliokuwa naye.”

127 Na tazameni. Musa alipokufa, akasimama juu ya mwamba huo. Mwajua nini kilitendeka? Biblia ilisema kuwa “Malaika” walikuja na wakamchukua.

128 Ni tofauti jinsi gani na yule kijana mwingine! Huyu kijana, oneni, alipokufa, hakuwa na ye yote wa kumshika, kwa hivyo yeye alizamia tu gizani, akaingia kuzimuni, naye yuko kule sasa, mle.

129 Ndipo Musa alipoondoka maishani, alipoenda, yeye alikuwa amemchagua Kiongozi. Mama yake alimwongoza vema, baba yake alimfundisha vema. Ndiposa alipokua mkubwa, kijana, basi alisema, “Naona Uzima wa Milele, kama nikiandamana na maskini hawa, watu waliodharauliwa, na nienende nao, kwa sababu wao ni watu wa Mungu. Hainipasi. Ningekuwa mfalme, lakini sitaki kuwa mfalme. Naweza kuwa na pesa zote zilizoko Misri, kwa sababu nitazimiliki hizo. Sizitaki. Heri nienende na Yesu,” naye alipoenenda maishani mwote.

Ndiposa alipopiga hatua kuondoka maishani, yule kiongozi wake alikuwako kumshika mkono.

¹³⁰ Je, hamumtaki Kiongozi huyo? Je, hatumtaki Kiongozi huyo amshike kwa mkono wake?

¹³¹ Mamia ya miaka baadaye, yeye alionekana akiwa na Kiongozi wake mkuu. Yeye aliongoza. Yeye ali—alifanya chaguo, la ujana wake, na kwa hivyo basi Mungu alikuwa amemshikilia.

¹³² Mwajuaje? Yule tajiri yumo kuzimuni, huyo kijana tajiri aliyekataa. Mnaona, sasa kumbuka, yeye alikuwa na elimu, alikuwa na dini, alienda kanisani, alikuwa mtu mzuri, lakini alimkataa Yesu. Mwaona?

¹³³ Na kijana huyu alikuwa amelimishwa, naye alikuwa na dini, lakini yeye alimtaka Yesu. Oneni, Musa angekuwa tajiri zaidi ya—ya kijana huyu angalivyokuwa, kwa sababu yeye alikuwa na pesa, labda mashamba na mengineyo kama hayo, na labda siasa na kadhalika, lakini Musa angekuwa mfalme juu ya dunia. Naye aliacha hayo yote.

¹³⁴ Nanyi mwajuaje, watoto? Wakati Misri haitakuwako, na hazina hazimo, Musa atakuwako bado, kwa sababu yeye alichagua kitu sahihi. Mnaona? Yeye alichagua kitu sahihi kimwongoze.

¹³⁵ Wakati hakuna tena piramidi kubwa. Mmesoma kuhusu hizo piramidi za Misri? Mojawapo ya siku hizi, zitakuwa vumbi, chini ya bomu ya atomiki. Utajiri wote wa ulimwengu, watu watautupa hewani, na kulia, na kusema umekuwa vidonda miilini mwao, watalia na kuomboleza. Mnaona, vitakwisha.

¹³⁶ Lakini wale wanaomkubali Yesu kuwaongoza, hawatakufa kamwe. Wana uzima wa milele. Ijapokuwa wanakufa kawaida hapa, Yesu atawafufua tena.

¹³⁷ Yakupasa ufanye chaguo. Chaguo lako litaamua kituo chako cha Milele. Kumbuka, Yesu auliza kila mmoja wetu, “Nifuate ukitaka Uzima.” Unaona, uongozi, “Unifuate, na utakuwa na Uzima wa Milele.” Nami nina hakika, hata kwetu watu wazima, tumepata kitu fulani kwa haya, pia. Ukitaka uzima yakupasa ukubali. Ukitaka dini ukubali ukitaka. Kile kikupasacho kufanya, kile ukubalicho, hicho ndicho utapata. Lakini kwangu na kwenu, na kwa hawa watoto wadogo, kumbuka, una mwaliko. Yesu alisema, “Unifuate, na upate Uzima wa Milele.” Hilo ndilo tunalotaka kufanya, sivyo?

¹³⁸ Sasa wangapi wenu wanaotaka hakika kumfuata Yesu, na kusema, “Kutoka, kutoka, nitakapokuwa mkubwa kutosha na wa umri wa kutosha kufanya chaguo langu, na kufanya yale. . . Sijali nina pesa nyingi vipi, ni maskini vipi, vipi watu wanavyonichekelea, au cha chote kile, nataka kumfuata Yesu. Nataka kufanya chaguo la Musa, si la yule kijana tajiri?”

Wangapi wanataka kufanya hilo papa hapa? Sasa mnataka hakika kufanya hilo?

¹³⁹ Nawatakeni msimame pamoja nami. Nakutakeni uweke mkono wako juu ya moyo wako, na uuinue mkono wako wa kuume juu. Nakutakeni mfunge macho yenu sasa na mwinamishe vichwa vyenu, na msembe tu maneno haya nyuma yangu. [Makutano wanarudia kila fungu la maneno baada ya Ndugu Branham, katika ombi linalofuata—Mh.]

¹⁴⁰ Yesu mpendwa, ["Yesu mpendwa,"] Nayatoa maisha yangu kwako. ["Nayatoa maisha yangu kwako."] Nimesikia mahubiri haya, ["Nimesikia mahubiri haya,"] ambapo vijana wawili walifanya chaguo lao. ["ambapo vijana wawili walifanya chaguo lao."] Sitaki nifuate njia ya yule kijana tajiri mtawala. ["Sitaki nifuate njia ya yule kijana tajiri mtawala."] Lakini nataka kufuata njia ya Musa.

["Lakini nataka kufuata njia ya Musa."] Mimi bado ni mtoto. ["Mimi bado ni mtoto."] Niongoze, Yesu mpendwa, ["Niongoze, Yesu mpendwa,"] hata Uzima wa Milele. ["hata uzima wa milele."] Amina. ["Amina."]

Sasa inamisheni vichwa vyenu.

¹⁴¹ Yesu mpendwa, siku moja, katika safari zako hapa duniani walikuletea wewe watoto kama hawa kama ambao nimekuwa nikiwahubiria adhuhuri, hii. Na wanafunzi walisema, "Bwana amechoka sana. Yeye alihubiri asubuhi hii. Yeye alihubiri, haya na yale, naye amechoka sana. Msimsumbue."

¹⁴² Lakini, Yesu, ulisema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, kwa maana walio mfano wa hao, Ufalme wa Mbinguni ni wao."

¹⁴³ Bwana Mungu, leo pokea hawa watoto wavulana kwa wasichana hapa, katika hii shule ya haki, hapa ambapo ndugu yetu amekuja kando upande huu wa jangwa hapa, kuwaleta jamaa wanaotaka kujitenga wenyewe na mambo ya ulimwengu, kuwa wageni wako pekee. Na sasa watoto wao wako hapa, wakichunguza maisha ya baba na mama zao, kama tulivyo—kama tulivyo vielelezo katika yote tufanyayo. Ee Mungu mpendwa, Muumba wa Mbingu na nchi, ongoza miguu yetu, Bwana, kwamba hatutafanya lo lote mbele ya hawa watoto, ambalo lingewakwaza safarini mwao. Kwa kuwa imesemwa, ingefaa tufungiwe shingoni mwetu jiwe la kusagia na kutoswa baharini, kuliko kumkosesha mmojawapo wa wadogo hawa. Ulisema, "Malaika zao siku zote huutazama uso wa Baba Yangu aliye Mbinguni," yule Malaika mkuu, na Malaika mlinzi, juu ya kila mmoja wa nafsi hizi dogo.

¹⁴⁴ Walipoketi adhuhuri hii hali macho yao madogo yako wazi, wakitazama na kujibu maswali, na kusikiza hadithi za watoto wachanga za Biblia, jinsi hawa vijana wawili walikata kauli zao, na kila mmoja wao aliweka maisha yake Kwako. Ewe Yehova

Mungu, waongoze, walinde. Na wao wampate huyu Kiongozi mkuu, Yesu Kristo, atakayewaongoza wao wakati baba na mama na waalimu wamemaliza nao. Na uwaongoze hata Uzima wa Milele, kama ulivyofanya na Musa, kama ombi lao nyenyekevu, dogo, la watoto lilivyokuja wewe. Nakupa wao, Bwana, kama mtumishi wako, kama thawabu na kito cha taji yako. Watumie, Bwana, kukutukuza wewe, duniani. Katika jina la Yesu. Amina.

¹⁴⁵ Nanyi wadogo, watoto, mwaweza . . . Sasa mwajisikia vizuri sana kuhusu hayo sasa? Mwajua Yesu yuaenda kuwaongoza na kuwaonyesha njia. Je, mwaamini hilo? Na Yesu atawafanyeni ninyi wavulana wadogo kama tu Musa na Miriamu, yule nabii wa kike na nabii wa kiume, atawafanyeni ninyi watu wakuu.

¹⁴⁶ Sasa, sisi watu wazima, ambao tumemkubali, si tunataka yeye atuongoze sisi, pia? Namtaka yeye aniongoze, aongoze miguu yangu, aushike mkono wangu. Mwaona? Na hata nifikapo chini pale mtoni, ni—ninataka kuushika mkono wake. Sisi sote twataka hilo sivyo?

¹⁴⁷ Yesu mpendwa, tuongoze, pia, Baba. Sasa tunakaribia kuachana mmoja na mwingine. Yanipasa nirudi Tucson. Yanipasa nijitayarisha kwa mikutano inayokuja. Mungu, nakabidhi kundi hili la watu, Ndugu leo na Ndugu Gene, na wafuasi wote hapa, mikononi mwako, kuwa utawabariki na kuwapenda, ukiwasamehe maovu yao yote, ukiwaponya magonjwa yao yote, kuwaweka daima katika upendo na ushirika, na kuwatia moyo wale wange . . . choka. Na wakati mwingine huenda shetani angekuja na kuwavunja moyo, lakini, kumbuka, ulipitia katika mambo yayo hayo, kuvunjwa moyo kuachwa na—na watu wa ulimwengu huu, na watu. Na wakati mwingine marafiki wapendwa sana, hata kwa jamaa, tumekataliwa. Lakini kunaye mmoja ambaye tumemchagua. Yeye hatatupungukia wala kutuacha.

¹⁴⁸ Tuongoze, Bwana, kwa Uzima wa Milele. Naomba kuwa utatujalia haya: kwamba tunaweza kukusanyika pamoja wakati mwingi zaidi, duniani, na kunena juu yako na kuongea juu yako. Na ndipo katika siku hiyo kuu ulimwengu uishapo na wakati wote umefilia katika umilele, na tukakutane katika ufalme huo mkuu, kama jamaa isiyotengana, kuishi pamoja baadaye, milele. Tukubalie Bwana. Hata wakati huo, na tufanye kazi, tujishughulishe kwa nguvu zetu zote, huku jua lingali linaangaza. Kwa kuwa twaomba katika jina la Yesu. Amina.

¹⁴⁹ Mungu awabarikini kila mmoja wenu. [Nafasi tupu kwanye ukanda—Mh.]

Mungu awe nanyi daima,
Hata twonane ya pili;
Awachunge kwa fadhili, Mungu awe nanyi
daima.

Hata twonane huko juu,
Hata twonane kwake kwema;
Hata twonane huko juu,
[Asanteni, enyi watu.] Mungu awe nanyi
daima.

Mungu awabariki ninyi nyote.



UONGOZI SWA65-1031A
(Leadership)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Oktoba 31, 1965, kule Prescott, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org